# Kristo 9



Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


YUDEA KARIBU NA YORDANI.
YESU ALINDELEA KUFUNZA NA KUPONYA KWAKE.
NDIYE YULE.
TULIFANYE SASA?
ASANTE! ASANTE SANA!
HAKUNA SABABU KWA NINI TUSIFANYE.
MWALIMU! TUNA SWALI!
NDIO! JE NI HALALI MWANAMUME KUMTALIKI MKEWE?
KWA SABABU YOYOTE?
SIKIZENI KILA MTU!
SIKIZENI KWA MAKINI ANALOLISEMA MTU HUYU!
MUMESOMA SHERIA. MWAJUA.
HAPO MWANZO, MUUMBAJI ALIWAUMBA MUME NA MKE.
KWA SABABU HII WANAWAACHA WAZAZI WAO NA KUWA MWILI MMOJA.
SI WAWILI TENA, BALI MMOJA.
BINAADAMU HAFAI KUTENGANISHA ALICHOKIUNGANISHA MUNGU.







MATHAYO 19:7-14; MARKO 10:10-14; LUKA 18:15-16










MATHAYO 19:14-15; MARKO 10:14-16; LUKA 18:16-17






MATHAYO 19:16-20; MARKO 10:17-21; LUKA 18:18-22




MATHAYO 19:21-23; MARKO 10:21-23; LUKA 18:22-24






MATHAYO 19:23-28; MARKO 10:25-28; LUKA 18:24-28




MATHAYO 19:29-20:2; MARKO 10:29-31; LUKA 18:29-30


BAADAYE MTU YULE ALIENDA AKAPATA WATU WENGINE WATAFUTA KAZI.
ALIKUBALI KUWALIPA WAFANYE HADI MWISHO WA SIKU.
KISHA TENA NAADAYE ALIPATA WENGINE NA KUWAAJIRI.
KISHA TENA ALIPATA WENGINE.
KULIPOKUCHWA ALIKUWA NA WATU WENGI WANAMFANYIA KAZI.
ALIMWAMBIA MSIMAMIZI AWALIPE WAFANYA KAZI.
"KILA MMOJA, KUTOKA ALIYEAJIRIWA WA KWANZA MPAKA WALIOAJIRIWA MWISHO, WALILIPWA DINARI."
"WALIOAJIRIWA KWANZA WALIKASIRIKA."
"WALINUNG'UNIKA LAKINI MWENYE SHAMBA ALIWAULIZA:"
MLIKUBALI KUFANYIA DINARI MOJA, SIO? KWA HIYO ICHUKUE MUENDE!
NATAKA KUMPA WA MWISHO NILIYEMUAJIRI SAWA!
KWANI SINA HAKI KUFANYA NITAKACHO NA PESA ZANGU?
AMA MNA WIVU KWA SABABU MIMI NI MKARIMU?
KWA HIYO WA MWISHO ATAKUWA WA KWANZA.
NA KWANZA ATAKUWA WA MWISHO.




MATHAYO 20:17-19; MARKO 10:32-34; LUKA 18:31-34






MATHAYO 20:20-23; MARKO 10:35-39




MATHAYO 20:23-28; MARKO 10:40-45




MATHAYO 20:29-34; MARKO 10:46-52; LUKA 18:35-43


IMANI YENU IMEWAPONYA.
PATA KUONA.
YESU AKAENDELEA NA SAFARI YAKE.
PALE YERIKO MPYA.
MTOZA USHURU TAJIRI ALIYEITWA ZAKAYO ALITAKA KUMUONA YESU LAKINI HAKUWEZA.
WATU WENGI MNO.
SITAWAHI KUONA VIZURI KUWAPITA.
ISIPOKUWA...
KWA NINI?
SONGA KAFUPI!
KRAK
OOF!
SIO KAMA MTU YEYOTE AWEZA KUNIDHARAU ZAIDI!


KUNA NINI ZAKAYO?
MTOZA USHURU TAKATAKA HAWEZI KUONA JUU YA VICHWA YA WANAUME WA KWELI!
NIMESIKIA MENGI SANA KUMHUSU...
LAKINI KUMUONA!
ZAKAYO?
ZAKAYO SHUKA CHINI!
AAH, NDIO...NDIO BWANA...
YESU AWEZA KUWA ATAKA NINI NAYE?
KWANI HAJUI NI MTU AINA GANI?
AMEJUA JINA LAKE!




LUKA 19:4-5



BWANA... BWANA... RABI...NI...
WAHITAJI NINI TOKA KWANGU?
NAHITAJI KUKAA NYUMBANI MWAKO!
NDIO, NDIO! NJOO!
NJOO!
KWA NINI AKAE NYUMBANI MWA MWENYE DHAMBI KAMA ZAKAYO?
KWA NYUMBA YA ZAKAYO...
NAJUA WATU WANACHOKISEMA NA NI KWELI!
MTU KAMA WEWE HUPASWI KUWA NYUMBANI MWA MTU KAMA MIMI.
LAKINI--
--SITAKI KUWA "MTU KAMA MIMI"!
NATAKA KUWA MTU KAMA WEWE!
BWANA NITAPEANA NUSU YA MALI YANGU KWA MASIKINI!
NA NITAMLIPA MARA NNE YEYOTE NILIYEMDANGANYA!
NAFIKIRIA TWAMUONA NGAMIA AKIPENYA KWENYE TUNDU LA SINDANO!
KWA MUNGU YOTE YAWEZEKANA!
KWA KWELI UFALME WA MUNGU UMEKARIBIA!
UKOMBOKOZI UMEKUJA NYUMBANI MWA MTU HUYU LEO.
KWA SABABU ZAKAYO, KAMA NYOTE HAPA, NI MWANA WA IBRAHIMU!
HICHI NDICHO MWANA WA ADAMU AMEKUJA KUKIFANYA!
KUTAFUTA NA KUOKOA KILICHOPOTEA!


WATU WENGI WANADHANIA UFALME WA MUNGU UTATOKEA TU.
LAKINI ACHA NIWAAMBIE HADITHI...
MTU MTUKUFU WA KIFALME ALIKUWA ANAENDA KUFANYWA MFALME.
ALIWAITA WATUMISHI WAKE KABLA HAJAONDOKA.
ITUMIE NA KUIWEKEZA VIZURI MPAKA NIRUDI.
NAWAPA KILA MMOJA WENU MINA.
WATUMISHI HAWA HAWAKUTAKA AWE MFALME LAKINI WALIFANYA ALIVYOSEMA.
ALIRUDI BAADA YA KUPEWA UFALME.
BWANA, NILIPATA MINA KUMI TOKA ILE ULIYONIPA.
VYEMA SANA MTUMISHI MUAMINIFU!
UMEKUWA MUAMINIFU KWA JAMBO DOGO KWA HIYO NITAKUPA MAMLAKA KWENYE MIJI KUMI!
BWANA, NIMEPATA MINA TANO KWA ZILE ULIZONIPA.
UMENIONYESHA NAWEZA KUKUAMINI.
NAKUPA MAMLAKA KWENYE MIJI MITANO!
BWANA, NAJUA WEWE NI MTU MGUMU KWA HIYO NILIKICHUKUA ULICHONIPA NA KUKIFICHA KANDO.
NDIO HII.
WEWE MTUMISHI MUOVU! KAMA ULIJUA MIMI NI MTU MGUMU INGEFAA UJUE NINATARAJIA ZAIDI YA HIVI!




LUKA 19:23-28; YOHANA 12:1,9,11, 17-18






YOHANA 11:57; 12:10-11, 19




MATHAYO 21:1-6; MARKO 11:1-6; LUKA 19:29-34






MATHAYO 21:7; MARKO 11:6-7; LUKA 19:35; YOHANA 12:14




MATHAYO 21:7; MARKO 11:6-7; LUKA 19:35




MATHAYO 21:8-9; MARKO 11:8-10; LUKA 19:36-38; YOHANA 12:12-13




MATHAYO 21:4-5; YOHANA 12:12-16


MWANA WA DAUDI AMEBARIKIWA!
HOSANNA!
"HOSANNA"? "TUOKOE BWANA."
WANAMLETA AWAOKOE?
MUONE AKIINGIA MJINI!
WATU WAFANYA NI KAMA YEYE NI MFALME!
UNASHANGAA?
KAMA UNGEONA TULIYOYAONA--
--KUSIKIA NA KUONA WALICHOKISIKIA NA KUKIONA WATU HAWA--
--MUNGEPUNGA MATAWI HEWANI NA KUZIWEKA NGUO ZENU CHINI YA MIGUU YA PUNDA PIA!
HOSANNA!
HOSANNA!



LUKA 19:39


MWALIMU!!!
WAKASHIFU!
WAKASHIFU WANAFUNZI WAKO!
WAKASHIFU WAFUASI WAKO!
WANALETA VURUGU AJABU!
NA VITU WANAVYOVISEMA--
HAMJUI MNACHOKIULIZA.
HAWA WATU WAKINYAMAZA MAWE YATALIA.
NJOONI.
HAKUNA HAJA.
KAMA TU MUNGELIJUA.
MUNGELIJUA KINACHOKUJA SIKU HII JERUSALEMU.
AMANI YENU.
LAKINI IMEFICHWA KUTOKA MACHONI MWENU.
LUKA 19:39-42



SIKU YAJA WAKATI MAADUI WATAWAVIRINGA.
KUWAZINGIRA TOKA PANDE ZOTE.
WATAWAPIGA NYINYI NA WANA WENU HADI KWA ARDHI.
NA WATAFANYA HIVI NDANI YA KUTA ZIZI HIZI!
HAKUNA JIWE HATA MOJA LITABAKISHWA JUU LA JENGINE.
NA HAYO YOTE SABABU HAMKUTAMBUA MUNGU ALIPOWAJIA.
YESU ALIENDA HEKALUNI USIKU HUO NA WATU ZAIDI WAKAMUONA.
LAKINI ILIKUWA USIKU SANA, YEYE NA WALE THENASHARA WAKARUDI BETHANIA.
NA JUMAPILI YA JUMA HIYO YA MWISHO IKAISHA.




LUKA 19:43-48


TULIKAA NJE YA YERIKO YA KALE KILA SIKU.
ASUBUHI KULIKUWA BARIDI NA KIMYA NA ILIKUWA NADRA KUPEWA CHOCHOTE MAPEMA HIVYO.
HADITHI YA VIPOFU
"WASIOONEKANA"
INAKAA KUNA WATU ZAIDI YA KAWAIDA.
NDIO.
HII SI SAWA. WATU WENGI HIVI MAPEMA HIVI.
NA HAKUNA MASHILINGI YA KUONYESHA.
TULIANGALIANA MIMI NA BATIMAYO.
LAKINI BATIMAYO ALIKUWA MAKINI ZAIDI.
NA MWENYE UTHUBUTU...
JAMBO!
BATIMAYO, WAFANYA NINI?
SAMAHANI BWANA!
NINI KINAENDELEA? MBONA KUNA WATU WENGI?
YULE MNAZARETI, YESU, YUAJA HIVI.
YESU?
KWELI?
BATIMAYO. SAA ZENGINE ANA MDOMO SANA.


UMESIKIA?
YESU! MNAZARETI!
NDIO.
WAJUA HII YAMAANISHA NINI?
LA.
YEYE NDIYE! WANAYEMUITA MWANA WA DAUDI!
WAJUA YAMAANISHA NINI?
AAAH
NINI BATIMAYO?
YEYE NI MASSIAH!
ALIYEKUWA AKIPONYA WATU NA KUFUKUZA MAJINI NA KUBATIZA!
KWA HIVYO?
KAMA NI MKUU NA MWENYE NGUVU UNAVYOSEMA, HATASIMAMA KUWASAIDIA VIPOFU WAWILI.
HATA HATATUONA KWENYE UMATI!
HATUONI LOLOTE LAKINI BADO TUNAJUA VITU, SIO?
BATIMAYO, WAFANYA NINI?
WAPANGA JAMBO. NINAJUA KUTOKA KWA SAUTI YAKO.
SAUTI YANGU! KABISA!


YESU!
YESU, MWANA WA DAUDI!
NIREHEMU!!!
BATIMAYO! TAFADHALI!
UNATUFANYA TUWE KITU CHA AJABU!
NDIO, NI KUSUDI!
YESU!!!
WANISIKIA?
TUREHEMU!
BATIMAYO, WACHA. TAFADHALI.
KWA NINI?
KUNA HATARI GANI?
ANAWEZA KUTUPONYA!
NA UNA WASIWASI WATU WATAFIKIRIA NINI!
WAJUA NINI? WATU TAYARI WANATUONA WASUMBUFU!
ASIPOTUSIKIA WATU WATADHANIA TU WASUMBUFU KULIKO KAWAIDA TU!
YESU!
YESU, MWANA WA DAUDI!


TUREHEMU!
NDIO!
NI HIVYO!
YESU!
MWANA WA DAUDI!
TUREHEMU!
YESU!
*YESU!!!*
TUSIKIE! TAFADHALI! TUREHEMU!
WE, NYAMAZA!
TAFADHALI! MWANA WA DAUDI!
PIA SISI NI WANA WA IBRAHIMU!
NYAMAZA!


YESU!
FUNGENI MIDOMO YENU!
YESU!
YESU, MWANA WA--
JAMANI, NYAMAZENI!
YESU HAITAJI WATU KAMA NYINYI KUPIGA KELELE!
LABDA WANENA UKWELI BATIMAYO.
YESU HANA SABABU YA KUTUSIKIZA SISI.
NDIO. ANAYO.
ATATUSIKIZA KWA SABABU YEYE NDIYE.
YESU! MWANA WA DAUDI!
TAFADHALI! TUREHEMU!
MBONA MSINYAMA--
WALETENI KWANGU!
--HAYA.
NJOO BWANA, AWAITA.
ATUITA SISI?
NDIO! ALITUSIKIA TUKIMUITA!


YUKO WAPI?
NIKO HAPA.
MWATAKA NIWAFANYIE NINI?
BWANA.
RABI.
TWATAKA KUONA.
TAFADHALI YESU.
WAWEZA, SIO?
NDIO. POKEA KUONA KWENU.
IMANI YENU IMEWAPONYA.
WATU WENGI WALITUPUUZA TULIPOKAA MAHALI PALE.
WATU WENGI HAWAKUONA.
ASANTE!
AH, ASANTE!
LAKINI ALITUSIKIA. ALITUONA.
NA TULIWEZA KUONA!
BATIMAYO. SAA ZENGINE ANA MDOMO SANA.
NA NINAFURAHIA ALIKUWA.

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."













**SUPERBIBLE.TV**